# FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA VITUO ATAMIZI VYA AIC

Kabla ya kujaza fomu, soma maelezo kuhusu sifa za muombaji, masharti ya kuomba na jinsi ya kujaza na kuwasilisha fomu iliyopo chini.

- Sifa za Kijana zinazotakiwa: Ueledi wa ujasiriamali, elimu/maarifa, mwenye uzoefu kwenye kilimo na kilimobiashara, awe na tabia njema, utii, nidhamu, mchapa kazi, fikra chanya, mwa  minifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa kike wanapewa kipaumbele.

- Fomu ya maombi zinatapatikana kwenye tovuti za AIC (www.aic.co.tz) na PASS (www.pass.or.tz),   SUA-SAEBS, ofisi zote za PASS za Kanda na  ofisi za AIC (SUA, Morogoro na Taliri Farm Mbande, Kongwa).

- Ada ya fomu ni shs 10,000/-; na ada hiyo ilipwe kwenye akaunti ya PASS, benki ya CRDB.

    - Namba ya Akaunti: **01J1076972802**
    - Jina la Akaunti: **Private Agricultural Sector Support**
    - Tawi: **Morogoro**
    - Taja jina lako ikifuatiwa na jina la kituo atamizi unachoomba kwenye kumbukumbu ya malipo (Pay in slip); **kwa mfano: 'Paul John – AIC Kongwa' au 'Paul John – AIC Morogoro'**

- **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/06/2020 saa 11.00 jioni.**

- Mchakato wa maombi utajumuisha: Kujaza fomu, kulipa ada, na kuwasilisha fomu pamoja na kumbukumbu ya malipo kwa PASS AIC.

- Baada ya PASS AIC kupokea fomu; Watachaguliwa vijana 280 kushiriki kwenye mafunzo/mchujo wa siku 5, ikiwemo siku moja ya kutahiniwa na kuhojiwa. Hatua ya mwisho ya mchakato baada ya mafunzo ni kuchaguliwa kwa vijana 100 wataka ojiunga na kituo atamizi cha Morogoro na vijana 40 watakaojiunga na kituo atami zi cha Kongwa kwa muda wa miezi 12 kuanzia Oktoba 2020 hadi Septemba 2021

- Mchakato wa uchaguzi utafanyika Morogoro kwa wale wanaoomba kujiunga na kituo atamizi cha mboga na matunda cha SUA-AIC Morogoro na kwa wale wanaoomba kujiunga na kituo atamizi ya unenepeshaji wa mbuzi na usindikaji wa nyama cha AIC Kongwa, mchakato utafanyika Kongwa, Dodoma na kila kijana atakayeshiriki kwenye mchakato huo atajikimu kwa gharama zake binafsi (nauli, malazi na chakula) kwa muda wa siku 5.

- Unaweza kutuma fomu kwa baruapepe kwenda: **maombi@aic.co.tz,** au kwa kupel eka kwenye ofisi ya AIC Morogoro na Mbande, Kongwa, na ofisi za PASS iliyopo karibu nawe.

- Angalizo: Usiambatanishe maelezo hayo hapo juu unaporudisha fomu. Rudisha fomu iliyojazwa na fomu ya muhamala wa malipo ya benki.

## FOMU YA MAOMBI VITUO ATAMIZI VYA AIC

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Jina | | | | | |
| 2 | Barua pepe na Simu | | | | | |
| 3 | Weka **Tiki sehemu moja tu** Kituo Atamizi unachoomba | Mbogа na Matunda Morogoro | | Unenepeshaji wa Mbuzi na Usindikaji wa Nyama, Kongwa | | |
| 4 | Anwani, Wilaya na Mkoa | S.L.P Wilaya Mkoa | | | | |
| 5 | Umri na jinsia (Mme au mke) | Umri Jinsia | | | | |
| 6 | Hadhi ya Ndoa (chagua moja) | Sijaoa / Nimeoa-olewa / Nimeachika / Mjane / mengineyo | | | | |
| 7 | Elimu yako na mwaka uliohitimu | Elimu Mwaka | | | | |
| 8 | Kama ni Chuo (kozi uliyosoma) | | | | | |
| 9 | Jina la Chuo | | | | | |
| 10 | Eleza maarifa na uzoefu wako kwenye kilimo/ufugaji? | | | | | |
| 11 | Eleza maarifa na uzoefu wako kwenye ujasiriamali? | | | | | |
| 12 | Eleza kwa ufupi shughuli kuu ya kiuchumi (inayokuingizia kipato) unayofanya kwa sasa? | | | | | |
| 13 | Kwa nini unataka kujiunga na Kituo Atamizi cha PASS AIC? (Toa maelezo) | | | | | |